

Uchanganyaji Msimbo katika Jamii lugha za Mitandaopepe: Mtagusano wa Kiswahili na Kiingereza

Rhoda P. Kidami¹

Ikisiri

Mitandaopepe² imetoa fursa kwa watu kutagusana katika masuala anuwai ya kijamii. Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazotumiwa katika mitandaopepe, ndani na nje ya Tanzania. Kutokana na kukua na kusambaa kwa lugha hiyo ulimwenguni kote, kuna haja ya kuchunguza mwonekano wake katika muktadha huo wa kimawasiliano pepe. Lengo la makala hii ni kuchunguza jinsi Kiswahili kinavyotagusana na lugha ya Kiingereza katika mawasiliano hayo, hususani kwenye kipengele cha uchanganyaji msimbo. Data za utafiti huu ni maoni yaliyotolewa kwenye mtandao wa *YouTube* baada ya watu kusikiliza hotuba za Kiswahili za Mwalimu Nyerere. Jumla ya maoni elfu mbili na sitini yalikusanywa kutoka katika hotuba tatu. Uchanganuzi wa data hizo uliongozwa na Kiolezo cha Myers-Scotton (2001) kinachohusu lugha msingi na lugha changiaji katika kipengele cha uchanganyaji msimbo. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba lugha za Kiswahili na Kiingereza zinakamilishana katika muktadha wa kimawasiliano pepe. Katika muktadha tofautitofauti, lugha mojawapo imetumiwa kuwa msingi wa mawasiliano huku nyingine ikijaliza sarufi ya lugha msingi. Wakati mwingine, lugha zote mbili zimetumiwa kwa pamoja huku kila moja ikijikamilisha kisarufi.

1.0 Utangulizi

Lugha hutumiwa na watu kubadilishana mawazo, hisia na taarifa mbalimbali. Jamii inapokuwa na lugha nyingi, wakati mwingine watu hutumia lugha zaidi ya moja katika mawasiliano yao ambayo yanaweza kuwa katika mazungumzo au maandishi. Matumizi hayo ya lugha mbili au zaidi katika tamko au andiko moja, hufasiliwa kama uchanganyaji msimbo (Mabule, 2015; Yusnida, Muliawati na Rezeki, 2022). Aidha, dhana ya uchanganyaji msimbo huhusiana sana na

¹ Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Barua pepe: rhodapeterson@udsm.ac.tz; kidamis@yahoo.com

² Haikutumiwa 'mitandao ya kijamii' kama ilivyozoeleka kwa sababu ni dhana pana inayohusisha majukwaa ya kidijiti (k.v. *Facebook* na *Twitter*) na yasiyo ya kidijiti (k.v. mikusanyiko ya kifamilia na matukio ya kijamii (Baumann na Utz, 2021).

dhana ya ubadilishaji msimbo. Uhamaji kutoka lugha moja hadi nyingine katika mawasiliano bila kuathiri sarufi ya lugha husika hufasiliwa kama ubadilishaji msimbo (Mustikawati, 2016; Tabe, 2023). Hata hivyo, lengo la makala hii sio kujadili uchangamani uliopo kati ya dhana hizo mbili. Uchanganyaji msimbo ni dhana jumuiishi inayohusisha mtagusano wa lugha ambao ndani yake kuna ubadilishaji msimbo. Watu wanapohama kutoka lugha moja na kutumia nyingine katika mawasiliano yaleyale, tayari kwa namna moja au nyingine wamechanganya msimbo (Harya, 2018). Uchanganyaji huo unaweza kujitokeza katika vipengele mbalimbali vya lugha, kama vile mofimu, maneno, virai, vishazi, sentensi, aya na hata vilongo (Waris, 2012). Hivyo basi, katika makala hii uchanganyaji msimbo umefasiliwa kuwa ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika tamko au andiko moja. Uchanganyaji huo unaweza kujitokeza ndani au nje ya sentensi ilimradi hakuna mabadiliko ya mada katika mawasiliano husika.

Ingawa uchanganyaji msimbo unaweza kutokea kisdafa katika mawasiliano, tafiti mbalimbali zinadhihirisha kwamba kuna sababu anuwai za watu kuchanganya msimbo wanapozungumza au kuandika. Miongoni mwazo ni kutumiwa kama mbinu ya kufundishia na kujifunzia darasani (Shartiely, 2016), kujitambulisha kama mshiriki wa kundi fulani la kijamii (Mabule, 2015), kukosa msamiati katika lugha mojawapo au kufanya mawasiliano kuwa ya siri (Waris, 2012; Harya, 2016; Meliani, Ratminingsih na Mahendrayana, 2021), ufahari kwamba mhusika ana kiwango cha juu cha elimu (Radhaswati na Nitiasih, 2022), kurejelea nukuu za watu wengine (Yusnida, Muliawati na Rezeki, 2022), na utambulisho wa kiutamaduni na kitaifa (Tabe, 2023).

Mawasiliano kupitia mitandaopepe yameongezeka ulimwenguni kutokana na maendeleo ya matumizi ya intaneti na teknolojia ya vifaa vya kidijiti, kama vile simujanja, vishikwambi na kompyuta. Mawasilianopepe hayo yamewezesha watu kuandaa, kusambaza na kupokea taarifa mbalimbali kwa urahisi na kwa haraka zaidi. Kwa mfano, picha mnato au jengevu zinaweza kusambazwa kwa hadhira kubwa ulimwenguni ndani ya sekunde moja (Bridges, 2016; Saragih na Harahap, 2020; Alzubi, 2022). Aidha, taarifa hutolewa kwa namna tofautitofauti katika mitandaopepe, kama vile kwa kutumia maandishi, sauti na picha ambazo zinaweza kuwa za mnato au jengevu (Meliani, Ratminingsih na Mahendrayana, 2021). Kwa kutumia mitandaopepe, kama vile *YouTube*, *WhatsApp*, *Twitter*, *Instagram* na *Facebook*, watu wamepata fursa ya kutagusana katika masuala anuwai ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hatimaye, mtagusano huo umewezesha kuundwa kwa jamiilugha za kimtandao. Jamiilugha hizo zinaweza kuundwa na watu wenye uhusiano uliojengeka kutokana na jambo fulani linalowaunganisha, kama vile kusoma, kufanya kazi ama kuabudu pamoja. Vilevile, jamiilugha za kimtandao zinaweza kuundwa na watu wasiofahamiana kabisa bali huunganishwa na jambo au mada iliyowasilishwa na kujadiliwa mtandaoni (Landert, 2017; Rutechura, 2018; Kim na wenzake, 2021).

Mada mbalimbali za kisiasa, hususani za watu maarufu, hupakiwa mitandaoni na kuibua mijadala kadha wa kadha. Matalani, hotuba za Kiswahili za Mwalimu Nyerere zimepakiwa kwenye mitandaopepe ya *YouTube*, *WhatsApp* na *Facebook* na kuibua mijadala ya kisiasa. Hotuba hizo zimekuwa kivutio kwa watu kuzisikiliza katika maeneo tofautitofauti ulimwenguni. Mvuto huo umesababishwa na umaarufu wa Mwalimu Nyerere kutokana na mchango wake wa kisiasa nchini Tanzania na kwa baadhi ya nchi za bara la Afrika. Kwa mfano, kiongozi huyo alishiriki katika harakati za kuikomboa Tanzania kutoka kwa wakoloni. Vilevile, alishiriki katika ukombozi wa kisiasa wa nchi zingine za Afrika, kama vile Msumbiji na Afrika Kusini (Chacha, 2002; Sanga, 2020; Fedeo, 2021). Halikadhalika, hotuba za Nyerere za Kiswahili husikilizwa na watu wengi kutokana na kuwa Kiswahili ni lugha iliyosambaa na kupendwa na watu wengi ulimwenguni kote (Kandagor, 2020). Hivyo, hotuba hizo huwaunganisha watu kutoka maeneo tofauti ulimwenguni ambao baada ya kuzisikiliza hutoa maoni yao kwa njia mbalimbali, ikiwamo ya maandishi. Swali tunalojiuliza ni kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yana sura gani katika muktadha huo wa kimtandao unaotagusanisha jamii za maeneo tofauti ulimwenguni, hususani katika kipengele cha uchanganyaji msimbo?

Ingawa hotuba za Mwalimu Nyerere hupakiwa katika mitandao kadha wa kadha, utafiti huu uliangazia hotuba za Kiswahili zilizopakiwa kwenye mtandaopepe wa *YouTube*. Sababu za kujielekeza katika mtandao huu ni kutokana na umaarufu wake wa kusambaza taarifa kwa haraka kwa njia ya video. Tunaweza kusema kwamba *YouTube* ni jukwaa la kijamii ambalo watu hushirikishana habari kwa njia ya video (Strangelove, 2010; Shiryayeva na wenzake, 2020). Katika mchakato wa upakiaji video kwenye mtandao huo, lugha hutumika kufafanua vipengele mbalimbali, kwa mfano, kutambulisha na kufafanua picha na video zilizopakiwa. Pia, watazamaji wa picha na video husika huweza kutoa maoni yao kwa kutumia lugha. Kwa ujumla, lugha hutumiwa mtandaoni kushirikishana habari na taarifa mbalimbali.

Matumizi ya lugha katika mitandaopepe yametawaliwa na wingilugha kutokana na uchangamani wa jamiilugha za kimtandao. Tafiti zilizotangulia zinadhihirisha kwamba kuwapo kwa wingilugha kunasababisha uchanganyaji msimbo kuonekana kuwa hali ya kawaida katika mitandaopepe. Lugha zaidi ya moja hutumiwa katika mawasiliano kutokana na uchangamani wa jamiilugha hizo ambazo huhusisha watu wenye tajiriba tofauti za kimaeneo na pia viwango tofauti vya umahiri wa lugha (Mabule, 2015; Radhaswati na Nitiasih, 2022). Kwa kuwa jamii na lugha ni vipengele vinavyohusiana kwa karibu, jamii zinapochangamana, lugha za jamii hizo huchangamana pia. Hivyo, lengo la makala hii ni kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili inavyotagusana na lugha zingine katika jamiilugha za kimtandao, hususani Kiingereza. Mwelekeo umekuwa uchanganyaji msimbo wa Kiswahili na Kiingereza kwa sababu Kiingereza kinafasiliwa kuwa lugha anzilishi na inayotawala mawasiliano (Jagero, Mohochi na Indede, 2013; Crystal, 2008

katika Mnenuka, 2024). Halikadhalika, Kiingereza ni lugha inayotumiwa kwa mawasiliano katika nchi nyingi ulimwenguni (Plonski, Teferra na Brady, 2013). Kutokana na Kiingereza kunasibishwa na mawasiliano pepe, hata baadhi ya majina ya mtindo wa lugha unaotumika katika muktadha huo yameundwa kwa kuhusisha lugha hiyo ya Kiingereza, mathalani, ‘*netlish*’ na ‘*weblish*’. Jina ‘*netlish*’ limeundwa kwa kuunganisha baadhi ya herufi za maneno mawili ya Kiingereza ambayo ni *network* (mtandao) na *English* (Kiingereza). Kwa mtindo huohuo, jina *weblish* limeundwa kwa kuunganisha baadhi ya herufi za maneno *website* (tovuti) na *English* (Kiingereza) (Abusa’aleek, 2015; Monderin na Go, 2021). Majina haya ya lugha za mawasiliano pepe yanadokeza jinsi ambavyo matumizi ya lugha mtandaoni yalianza kunasibishwa na lugha ya Kiingereza.

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu matumizi ya lugha katika mawasiliano pepe. Mitindo ya lugha inayotumiwa katika mawasiliano pepe hayo imepewa majina tofautitofauti, kama vile ‘mazungumzo mtandao’ (Crystal, 2006), ‘lugha tandawazi’ (Mutembei, 2011; Faki 2018; Abdallah, 2018; Ndekiro, 2020), lugha za kidijitali (Benard, Kandagor na Opijah, 2017) na ‘lughapepe’ (Mnenuka, 2019). Baadhi ya tafiti zinadhihirisha kwamba ingawa mawasiliano pepe hufanywa kimaandishi, huambatana na sifa za kimazungumzo, mathalani, udondoshaji wa sauti na silabi katika maneno pamoja na matumizi ya msamiati usorasmi (Jagero, Mohochi na Indede, 2013). Sifa zingine za mawasiliano pepe ni matumizi ya namba kuwakilisha silabi, ufupishaji wa maneno, uchanganyaji msimbo na matumizi ya emoji na alama bunifu ambazo hazitumiki kwenye maandishi ya kawaida (Mutembei, 2011; Ndekiro, 2020; Mnenuka, 2024). Mawasiliano pepe yameibua mtindo mpya wa mawasiliano ambao hujumuisha nduni za maandishi na za kimazungumzo (Crystal, 2006; Benard, Kandagor na Opijah, 2017; Monderin na Go, 2021).

Mtindo huo wa mawasiliano katika muktadha wa kidijitali unadaiwa kuwa na athari hasi katika maendeleo ya lugha sanifu. Mathalani, Kiswahili sanifu kimeathiriwa na mawasiliano pepe katika vipengele vya uchanganyaji msimbo na uandishi usio kubalifu. Kutokana na athari hizo hasi, maoni yanatolewa kwamba vyombo vya kudhibiti matumizi hayo ya lugha vianzishwe (Faki, 2018; Abdallah, 2018; Ndekiro, 2020). Kwa upande mwingine, Crystal (2006) anasema kwamba matumizi ya lugha hubadilika ili kuendana na muktadha. Kwa kuwa muktadha wa kidijitali ni tofauti na miktadha mingine, hata matumizi ya lugha hayana budi kutofautiana. Maoni ya Crystal (2006) yanaungwa mkono katika makala hii. Kuelewa mitindo mbalimbali ya lugha katika jamii na kuitumia kutegemeana na miktadha husika ni jambo muhimu.

Vilevile, kuna tafiti mbalimbali zilizogusia jinsi uchanganyaji msimbo katika mawasiliano pepe unavyohusisha Kiswahili na lugha zingine. Msovela (2017) amechunguza ruwaza za ubadilishaji msimbo katika mawasiliano sogozi mtandaoni kwa kutumia mifano kutoka mtandao wa *Jamii Forum*, nchini Tanzania. Lugha zilizobainika kutumiwa kwa kuchanganywa ni Kiswahili na

Kiingereza. Uchanganyaji huo umedhihirika kuwa katika ruwaza mbili; ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi na ubadilishaji msimbo nje ya sentensi. Ubadilishaji msimbo ndani hutokea ndani ya sentensi ilhali ubadilishaji msimbo nje hujitokeza kati ya sentensi moja na nyingine. Katika mawasiliano hayo sogozi, Kiswahili kimetumiwa kama lugha msingi huku vipashio mbalimbali vya Kiingereza vikipachikwa katika sarufi ya Kiswahili. Naye Shoo (2019) amechunguza uchanganyaji wa lugha katika mawasiliano yanayofanywa na vijana wa vijijini nchini Tanzania kwa kutumia vifaa vya kielektroniki. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha uchanganyaji wa Kiswahili, Kiingereza na lugha za kikabila. Aidha, lugha za kikabila zimedhihirika kutumiwa kwa nadra sana kutokana na ukosefu wa maarifa ya kimaandishi ya lugha hizo.

Utafiti mwingine ni wa Dzahene-Quarshie na Sosoo (2023) ambao wamechunguza mbinu zinazotumiwa kuchanganya msimbo katika matangazo ya makampuni ya simu yanayorushwa katika mitandao ya *YouTube* na *Facebook* nchini Tanzania. Utafiti huu unaonesha kwamba kuchanganya Kiswahili sanifu, Kiingereza na Kiswahili cha mtaani ni hali ya kawaida katika matangazo ya mashirika ya simu (Airtel, Tigo³ na Shirika la Mawasiliano Tanzania) nchini Tanzania. Mbinu zilizobainika kutumiwa ni kama za Shoo, yaani uchanganyaji msimbo ndani na nje ya sentensi. Pia, inaonekana uchanganyaji msimbo katika matangazo hayo hautokei kwa ghafla bali umepangiliwa kwa umakini huku lugha msingi ikiwa Kiswahili sanifu.

Tafiti hizo zimeonesha jinsi Kiswahili kinavyotumiwa katika mawasiliano pepe, hususani kwa kuchanganywa na Kiingereza. Hata hivyo, tafiti hizo zimefanywa katika jamiilugha mtandao za makundi maalumu (kundi sogozi la *Jamii Forum*, rika la vijana wa vijijini na kundi la makampuni ya simu). Kiswahili ni lugha inayokua na kusambaa ulimwenguni kote, hatimaye, kutumiwa katika mitandaopepe mbalimbali ya kijamii (Kandagor, 2020). Lengo la makala hii ni kuchunguza mtagusano wa Kiswahili na Kiingereza katika jamiilugha changamani za kimtandao zinazohusisha watu wenye tajriba tofauti kirika na kimaeneo. Katika mtandao wa *YouTube*, baada ya video kupakiwa kila mtu yuko huru kutazama na kutoa maoni yake (Shiryayeva na wenzake, 2020). Hivyo, jukwaa hilo huunda jamiilugha mtandao yenye uchangamani wa watu mbalimbali.

Data za utafiti huu ni maoni yaliyotolewa na watu baada ya kusikiliza hotuba tatu (3) za Kiswahili zilizotolewa na Mwalimu Nyerere mnamo mwaka 1995 na kupakiwa kwenye mtandao wa *YouTube* kwa nyakati tofautitofauti. Hotuba ya kwanza ilihusu kiongozi anayefaa kuiongoza Tanzania⁴ na maoni yaliyokusanywa katika hotuba hii ni mia sita hamsini na tatu (653). Hotuba ya

³ Kuanzia Novemba 26, 2024 jina la Tigo limebadilishwa na kuwa Yas (<https://www.yas.co.tz/about/>)

⁴ Tanzania Yetu. (2021) *YouTube*. Maoni yalipakuliwa Septemba 14, 2022 kutoka <https://www.youtube.com/watch?v=jE7oTPXtpas>

pili ilihusu ushirikiano na mshikamano wa wafanyakazi.⁵ Maoni yaliyokusanywa ni mia mbili na tano (205). Hotuba ya tatu ilihusu kiongozi anayefaa kugombea kiti cha urais awamu ya tatu nchini Tanzania⁶ na maoni elfu moja mia mbili na mbili (1,202) yalikusanywa. Jumla ya maoni yote yaliyotumiwa kuwa data za utafiti huu ni elfu mbili na sitini (2,060). Maoni hayo yalikusanywa mwezi Septemba, 2022. Hotuba hizo zimehusishwa kwa sababu zimekuwa zikiwavutia watu wengi mtandaoni kutokana na maudhui yake, hatimaye kukidhi kigezo cha uteuzi wa sampuli kilichotumiwa katika utafiti huu. Kigezo hicho ni hotuba zilizokuwa na maoni yasiyopungua mia moja (100) wakati wa ukusanyaji wa data.

Baada ya data kukusanywa kutoka katika mtandao wa *YouTube*, zilichanganuliwa kwa kuongozwa na Kiolezo cha Uchanganyaji Msimbo cha Myers-Scotton (2001). Msingi wa kiunzi hiki ni kwamba uchanganyaji msimbo katika jamiilugha ulumbi huhusisha lugha msingi na lugha changiaji. Sarufi ya lugha msingi ndiyo inayotawala na kuongoza miundo ya lugha katika mawasiliano huku lugha changiaji ikisaidia kukamilisha vipengele vya kisarufi vya lugha msingi. Matalani, vipashio kama msamiati, virai na vishazi vya lugha changiaji huchopekwa katika miundo ya kisarufi ya lugha msingi. Kwa ujumla, lugha changiaji haitawali mawasiliano bali huwa kijalizo cha lugha msingi (Myers-Scotton, 2001). Kiunzi hiki kimetumiwa kuchunguza kipengele cha uchanganyaji msimbo kwenye maoni yaliyotolewa na watu baada ya kusikiliza hotuba za Kiswahili za Mwalimu Nyerere. Maoni yote elfu mbili na sitini (2,060) yalipitiwa ili kubainisha vipengele mbalimbali vya uchanganyaji msimbo. Mwelekeo ulikuwa kuaua Kiswahili kinavyotagusana na Kiingereza mtandaoni. Kisha, upambanuzi wa lugha msingi na changiaji ulifanyika ili kubaini kama Kiswahili kimetagusana kwa nafasi ya lugha msingi ama changiaji. Sehemu inayofuata inadokeza kwa ufupi lugha zilizotumiwa katika utoaji wa maoni kama zilivyodhihirika katika mawasiliano pepepe yaliyochunguzwa.

2.0 Lugha Zilizotumiwa katika Utoaji wa Maoni

Baada ya watu kusikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere kwenye mtandao wa *YouTube*, wametoa maoni yao kwa kutumia lugha mbalimbali. Ingawa hotuba zimetolewa kwa Kiswahili, lugha zilizobainika kutumiwa katika utoaji wa maoni ni Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa. Mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 1 inadhihirisha matumizi ya lugha hizo:

⁵ TZ Trending. (2021) *YouTube*. Maoni yalipakuliwa Septemba 14, 2022 kutoka <https://www.youtube.com/watch?v=IrH0hV-wG7Y>

⁶ Joseph Mabina . (2021) *YouTube*. Maoni yalipakuliwa Septemba 14, 2022 kutoka <https://www.youtube.com/watch?v=GAEpisZ3Cuk>

Jedwali Na. 1: Lugha Zilizotumiwa katika Utoaji wa Maoni

Na.	Lugha	Mfano wa Maoni 7
i.	Kiswahili	Hapa Kenya huwa tunachagua akina nani hawa? Wote walafi hadi tunabakia kuachia Mungu tu. Hongera mwalimu.
ii.	Kiingereza	<i>What a great speech. We wish we had someone like you in Uganda (RIP).</i> (Hotuba nzuri sana. Tunatamani tungekuwa na mtu kama wewe Uganda).
iii.	Kiswahili na Kiingereza	<i>Always legendary never die much respect</i> (watu mashuhuri hawafi kamwe heshima kubwa) kwa baba wa taifa, Mungu aendelee kukulaza mahali pema.
iv.	Kifaransa	<i>Nous avons presque la même langue je comprends mieux</i> (Ni kama vile tuna lugha sawia, ninaelewa vizuri).

Chanzo: Uwandani (2022)

Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1, lugha za Kiswahili na Kiingereza zimetumiwa kutolea maoni kwenye mifano i-iii. Nayo lugha ya Kifaransa imetumiwa katika mfano iv. Kwa kurejelea mifano hiyo ya matumizi ya lugha, tunapata dokezo kwamba waliosikiliza hotuba za Nyerere wana umahiri wa lugha zingine zaidi ya Kiswahili. Haya yanathibitishwa na hoja kwamba hotuba ni za Kiswahili lakini maoni yametolewa kwa Kiswahili na lugha zingine. Pia, mifano katika Jedwali Na. 1 (i na ii) inadokeza kwamba watoamaoni wametoka nchi za Kenya na Uganda mtawalia. Hata hivyo, imekuwa vigumu kubaini utambulisho wa watoamaoni wote kwa sababu wengine hawakudokeza utambulisho wao. Pamoja na hayo, mifano hiyo michache inatudhihirishia kwamba maoni yametolewa na watu kutoka sehemu mbalimbali, ndani na nje ya Tanzania. Hivyo, ni dhahiri kwamba hotuba za Mwalimu Nyerere, hususani za Kiswahili, husikilizwa na watu kutoka maeneo tofautitofauti.

Aidha, lugha zilizotumiwa katika utoaji wa maoni zimedhihirika kuwa katika mitindo tofauti. Baadhi ya maoni yametolewa kwa kutumia lugha moja, kama vile katika Jedwali Na. 1(i, ii na iv) ilhali mengine yamehusisha uchanganyaji wa lugha zaidi ya moja, yaani uchanganyaji msimbo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1(iii). Pia, yamedhihirika matumizi ya lugha sanifu, isosanifu na wakati mwingine makosa mbalimbali ya kiuandishi. Matumizi haya ya lugha yanadokeza jinsi jamiilugha za kimtandao zilivyo changamani na kwamba hujumuisha watu wenye viwango tofauti vya ujuzi wa lugha. Hata hivyo, katika utafiti huu kipengele cha uchanganyaji msimbo ndicho kilichomakinikiwa kama kinavyodadavuliwa katika sehemu inayofuata.

⁷ Maneno yaliyowekwa kwenye mabano ni tafsiri. Tafsiri za Kiingereza-Kiswahili katika makala hii zimefanywa na mtafiti. Tafsiri ya *Google* imetumiwa katika tafsiri za Kifaransa - Kiswahili kisha walumbi wa lugha husika walitumiwa kuhariri.

3.0 Uchanganyaji Msimbo katika Maoni yaliyotolewa na Watu baada ya Kusikiliza Hotuba za Nyerere kwenye YouTube

Ingawa lugha mbalimbali zimedhihirika kutumiwa katika utoaji wa maoni, uchanganyaji msimbo umehusisha zaidi lugha za Kiswahili na Kiingereza. Kifaransa kimetumiwa kwa kiasi kidogo sana. Matumizi haya ya lugha yanabashirika kutokana na kuwa nchi za Kiafrika takribani ishirini na sita (26)⁸ zinaitumia lugha ya Kiingereza kama lugha rasmi huku nchi za Kiafrika takribani hamsini na tatu (53) zikiitumia lugha hiyo kwa mawasiliano. Matumizi ya Kiingereza barani Afrika yanaongezeka hata kwa nchi ambazo zilikuwa na wazungumzaji wengi wa Kifaransa, kama vile Kameruni na Shelisheli. Pia, lugha hii inazidi kukua kimatumizi katika nchi za Afrika Magharibi ikiwa mbadala wa lugha za Kifaransa na Kireno (Plonski, Teferra na Brady, 2013).

Kwa upande wa Kiswahili, watu binafsi pamoja na jamii mbalimbali kutoka pande tofautitofauti za dunia wamekuwa wakijifunza, mathalani, kutoka sehemu za Ulaya, Asia, Marekani na nchi mbalimbali za Afrika (Moshi, 2006). Matumizi hayo ya Kiingereza na Kiswahili yanatupa dokezo kwamba upo uwezekano mkubwa wa Kiswahili kutagusana na Kiingereza kwa sababu ni lugha zinazotumiwa ndani na nje ya bara la Afrika katika shughuli mbalimbali rasmi na zisorasmi. Hivyo basi, ingawa data zinadhihirisha kutagusana kwa Kiswahili na lugha zaidi ya moja, makala hii imeangazia data za Kiswahili na Kiingereza kwa sababu ndizo lugha zilizotamalaki katika utoaji wa maoni. Vipashio vya lugha hizo vimetumiwa kwa pamoja kuwasilisha ujumbe mbalimbali kuhusu uongozi wa Mwalimu Nyerere.

Tafiti zilizotangulia zinadhihirisha pia uchanganyaji msimbo wa Kiswahili na lugha zingine na kwamba umeathiri maendeleo ya Kiswahili sanifu. Maandishi ya Kiswahili sanifu yamekuwa yakiandikwa kwa kuchanganywa na maandishi ya lugha zingine, jambo linaloonekana kuwa athari hasi (Faki, 2018; Ndekiro, 2020). Pamoja na athari hiyo inayodaiwa kuwa hasi, katika utafiti huu uchanganyaji msimbo katika mawasiliano pepe umesaidia kugubua jinsi lugha ya Kiswahili inavyotagusana na lugha ya Kiingereza katika muktadha wa kidijiti. Mawasiliano pepe hutofautiana na mawasiliano yanayofanywa katika miktadha mingine isiyo ya kidijiti. Hivyo, sifa za mawasiliano hayo hazina budi kugubuliwa ili kuzitofautisha na miktadha mingine. Kwa ujumla, uchanganyaji wa lugha katika utafiti huu umedhihirika kuwa katika viwango tofautitofauti ambavyo ni mofimu, neno na sentensi.

⁸ Nchi hizo ni Botswana, Kameruni, Eritrea, Gambia, Ghana, Kenya, Lesoto, Liberia, Madagaska, Malawi, Morisi, Msumbiji, Namibia, Nijeria, Rwanda, Shelisheli, Siera Leoni, Somalia, Afrika Kusini, Sudani Kusini, Sudani, Uswazi, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe (Plonski, Teferra na Brady, 2013).

Matumizi hayo ya lugha yamefafanuliwa na kujadiliwa katika sehemu zinazofuata.

3.1 Uchanganyaji Msimbo katika Kiwango cha Mofimu

Data za utafiti huu zinadhihirisha matumizi ya maneno yaliyoundwa kwa mchanganyiko wa mofimu za Kiswahili na za Kiingereza. Aidha, sarufi ya Kiswahili ndiyo iliyotamalaki huku maneno ya Kiingereza yakitumiwa kama vijalizo. Mifano ifuatayo inadhihirisha kiwango hicho cha uchanganyaji wa lugha:

Jedwali Na. 2: Uchanganyaji wa Mofimu za Kiswahili na Kiingereza katika Maneno

Na.	Maoni kutoka <i>YouTube</i>	Kiswahili Kuchanganya Mofimu za Kiingereza	bila
i.	Huyu mzee kama kuna mtu <i>anignore</i> atakuwa na matatizo yake binafsi.	Huyu mzee kama kuna mtu anapuuzia atakuwa na matatizo yake binafsi.	
ii.	Kama bado <i>unaicheck</i> hii tujuane, haichuji.	Kama bado unaitazama hii tujuane, haichuji.	
iii.	Tumekumiss baba wa taifa letu.	Tumekukumbuka baba wa taifa letu.	
iv.	Udini, rushwa ... tuviogope kama ukoma ... JPM pambana ili <i>kuabolish</i> kabisa visionekane.	Udini, rushwa ... tuviogope kama ukoma ... JPM pambana ili kuondoa kabisa visionekane.	
v.	Hivi <i>anayedislike</i> ujumbe kama huu yuko timamu kweli?	Hivi asiyependa ujumbe kama huu yuko timamu kweli?	

Chanzo: Uwandani (2022)

Katika Jedwali Na. 2(i-v) hapo juu, maneno *anignore* (anapuuzia), *unaicheck* (unaitazama), *tumekumiss* (tumekukumbuka), *kuabolish* (kuondoa) na *anayedislike* (asiyependa) yameundwa kwa mofimu za lugha mbili. Maneno hayo yameanza na mofimu awali za Kiswahili kisha kujalizwa na maneno ya Kiingereza ambayo yametumiwa kama mashina. Uambatishaji wa mofimu za Kiswahili na Kiingereza umesababisha kuundwa kwa maneno changamani, yaani yenye mofimu za lugha mbili tofauti. Mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 3 inadhihirisha uundaji huo wa maneno.

Jedwali Na. 3: Uchanganyaji wa Mofimu za Kiswahili na Kiingereza katika Maneno

Na.	Neno	Mofimu (Viambishi)		
		Kiswahili		Kiingereza
i.	<i>anaignore</i>	a- -na-	Nafsi ya tatu umoja Njeo ya wakati uliopo	<i>-ignore</i> shina
ii.	<i>unaichack</i>	u- -na- -i-	Nafsi ya pili umoja Njeo ya wakati uliopo Kirejeshi cha mtendwa	<i>-check</i> shina
iii.	<i>tumekumiss</i>	tu- -me- -ku-	Nafsi ya kwanza uwingi Njeo ya wakati timilifu Kiambishi cha mtendwa	<i>-miss</i> shina
iv.	<i>kuabolish</i>	ku-	Kinominishi cha kitenzi	<i>-abolish</i> shina
v.	<i>anayedislike</i>	a- -na- -ye -	Nafsi ya tatu umoja Njeo ya wakati uliopo Kirejeshi cha mtenda	<i>-dis- -like</i> ukanushi shina

Chanzo: Uwandani (2022)

Mifano katika Jedwali Na. 3 inadhahirisha jinsi watoamaoni kwenye hotuba za Mwalimu Nyerere walivyochanganya msimbo katika kiwango cha mofimu (viambishi). Maneno katika Jedwali Na. 2(i-vi) yameundwa kwa kuanza na viambishi awali vya Kiswahili kisha kufuatiwa na mashina yaliyoundwa na maneno ya Kiingereza. Katika Jedwali Na. 3(ii), neno *anayedislike* limeundwa na viambishi awali vitatu vya Kiswahili (a-na-ye-) kisha kujalizwa na viambishi viwili vya Kiingereza, yaani kiambishi cha ukanushi (-dis-) pamoja na shina (-like). Matumizi hayo ya lugha yanadokeza kwamba lugha ya Kiswahili imetumiwa kama lugha msingi. Hali hii ni kutokana na kwamba sentensi zilizotumiwa ni za Kiswahili huku maneno machache yakiwa yameundwa kwa mchanganyiko wa mofimu za Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mofimu za Kiswahili ndizo zilizotawala katika maneno hayo changamani, kama vile viambishi vya nafsi, njeo, virejeshi, mtenda na mtendwa. Kiingereza kimetumiwa kujaliza sarufi ya Kiswahili kwa kupachika neno la Kiingereza katika sehemu ya shina. Kama ilivyojitokeza katika utafiti wa Mnenuka (2013), uchanganyaji huu wa mofimu umejitokeza katika vitenzi. Hali hii inaonesha kwamba lugha za Kiswahili na Kiingereza zimetagusana katika kiwango cha mofimu kupitia vitenzi.

3.2 Uchanganyaji Msimbo katika Kiwango cha Neno

Baada ya watu kusikiliza hotuba za Nyerere kwenye mtandao wa *YouTube*, wametoa maoni yao kwa kuchanganya maneno ya Kiswahili na ya Kiingereza

katika sentensi. Sentensi zilizotumika katika mawasiliano ni za Kiswahili huku maneno ya Kiingereza yakichopekwa katika sentensi hizo. Mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 4 inadhihirisha matumizi hayo ya lugha.

Jedwali Na. 4: Uchopekaji wa Maneno ya Kiingereza katika Sentensi za Kiswahili

Na.	Sentensi za Kiswahili zenye Maneno Kiingereza	Kiswahili bila Kuchanganya Maneno ya Kiingereza
i.	Mwaka huu ndio ninazaliwa kisha <i>legendary</i> ndio anahutubia.	Mwaka huu ndio ninazaliwa kisha shujaa ndio anahutubia.
ii.	Katika watu <i>talented</i> Tanzania ilipewa ni Julius na John	Katika watu wenye vipaji Tanzania ilipewa ni Julius na John
iii.	Huyu jamaa ni <i>genius</i> .	Huyu jamaa ana uwezo mkubwa kiakili .
iv.	<i>Why</i> uliacha Tanzania mapema?	Kwa nini uliacha Tanzania mapema?
v.	Japo hayupo duniani huyu mzee, hakika <i>message</i> zake zina ujumbe mzito.	Japo hayupo duniani huyu mzee, hakika jumbe zake zina ujumbe mzito.

Chanzo: Uwandani (2022)

Tukirejelea Jedwali Na. 4(i-v) tunaona kwamba watoamaoni wanatumia mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza katika kufafanua hisia zao kuhusu Mwalimu Nyerere. Ingawa sentensi zilizotumiwa ni za Kiswahili, maneno ya Kiingereza yamechopekwa katika sentensi hizo kuchanuza sifa chanya za Mwalimu Nyerere. Sifa hizo ni kwamba alikuwa shujaa (*legendary*), mwenye kipaji cha uongozi (*talented*) na mwenye uwezo mkubwa kiakili (*genius*). Katika Jedwali Na. 4(iv), neno la Kiingereza *why* (kwa nini) linatumiwa kuchanuza hisia kwamba ameondoka duniani ikiwa bado Watanzania wanamhitaji. Katika mfano wa v, ujumbe unawasilishwa kwamba ingawa hayupo duniani, bado ujumbe (*message*) zake ni faafu kwa jamii kupitia hotuba mbalimbali ambazo alizitoa. Katika mifano hiyo, Kiswahili kinadhihirika kuwa msingi wa mawasiliano kwa sababu muundo wa sentensi uliotumika ni wa Kiswahili. Lugha ya Kiingereza imetumiwa na watoamaoni kama lugha changiaji kwa kuchepeka neno mojawoja katika sentensi za Kiswahili. Kama anavyosema Kandagor (2020) kuwa lugha ya Kiswahili inasambaa na kukua ulimwenguni kote, muktadha wa mawasiliano pepepe unadhihirisha hayo. Kiswahili kuwa msingi katika muktadha huo ni ishara kwamba kinatawala baadhi ya miktadha ya mawasiliano yanayofanyika kidijiti.

Kwa upande mwingine, Kiingereza kimetumiwa kama msingi wa mawasiliano katika kiwango cha neno na Kiswahili kama kijalizo cha

mawasiliano hayo. Sentensi za Kiingereza zimetumiwa kutoa maoni kuhusu Mwalimu Nyerere kama inavyodhihirika katika mifano inayofuata katika Jedwali Na. 5:

Jedwali Na. 5: Uchanganyaji wa Maneno ya Kiswahili katika Sentensi za Kiingereza

Na.	Sentensi za Kiingereza zenye Maneno ya Kiswahili	Tafsiri kwa Kiswahili bila Kuchanganya na Kiingereza
i.	<i>Julius Kambarage Nyerere you were a hero</i> mzee.	Julius Kambarage Nyerere ulikuwa shujaa mzee.
ii.	<i>No one in Tanzania will put on his shoes. Missing you badly</i> baba.	Hakuna anayeweza kuvaa viatu vyake katika Tanzania. Tunakukumbuka sana baba.
iii.	<i>Rest in peace</i> baba.	Pumzika kwa amani baba.
iv.	<i>We miss you</i> mzee <i>love from Uganda.</i>	Tunakukumbuka mzee Uganda tunakupenda.
v.	<i>Watching in 2021 and admiring</i> hapa Kenya.	Tunaitazama katika 2021 na inatuvutia hapa Kenya.

Chanzo: Uwandani (2022)

Lugha kuu ya mawasiliano iliyotumiwa katika mifano ya Jedwali Na. 5(i-v) ni Kiingereza. Sentensi za lugha hiyo zimetumiwa kuelezea sifa za Mwalimu Nyerere kwamba alikuwa shujaa (*hero*) na kwamba hakuna anayeweza kuongoza kama alivyotenda yeye nchini Tanzania. Kutokana na uongozi wake kukubalika kwa wengi, zinachanuzwa hisia kwamba anakumbukwa (*missing you*), hivyo, kumwomba apumzike kwa amani huko aliko. Pia, uongozi wake unakumbukwa na kutamaniwa hata nje ya Tanzania, yaani Kenya na Uganda. Katika sentensi hizo, sarufi ya Kiingereza ndiyo iliyotawala huku maneno ya Kiswahili yakitumiwa kukamilisha mawasiliano hayo ya Kiingereza. Matalani, maneno ya Kiswahili ‘**mzee, baba na hapa**’ yamepachikwa katika sentensi za Kiingereza kukamilisha miundo ya sentensi hizo. Mifano hiyo inadhihirisha jinsi Kiingereza kilivyotumiwa kama lugha msingi katika utoaji wa maoni huku Kiswahili kikitumiwa kama lugha changiaji.

Katika mawasiliano pepe, lugha za Kiswahili na Kiingereza zimedhihirika kutumiwa kwa pamoja huku kila lugha ikijikamilisha kisarufi, hususani katika kiwango cha neno. Hivyo, lugha zote mbili kuwa lugha msingi kwa wakati fulani na lugha changiaji kwa wakati mwingine. Matumizi hayo ya lugha yanatupa dokezo kwamba wapo wanajamiilugha za kimtandao wenye uelewa wa lugha hizo kiasi cha kuwa na uwezo wa kuzitumia kwa kuzichanganya kwa viwango vinavyofanana. Uchanganyaji huu wa lugha unawezekana kwa sababu lugha za Kiingereza na Kiswahili zina mawanda mapana ya kimatumizi ulimwenguni. Aidha, matokeo haya yanatofautiana na ya Msovela (2017) ambayo yanaonesha kuwa Kiswahili kilibainika kuwa msingi

wa mawasiliano sogozi katika mtandao wa *Jamii Forum*. Hata hivyo, kundi hili ni maalumu katika jukwaa lililosajiliwa tofauti na jamiilugha mtandao changamani katika jukwaa la *YouTube*.

3.3 Uchanganyaji Msimbo katika Kiwango cha Sentensi

Data zilizokusanywa kwenye mtandao wa *YouTube* zimedhihirisha matumizi ya uchanganyaji wa lugha kati ya Kiswahili na Kiingereza katika kiwango cha sentensi. Sentensi za lugha hizo zimetumiwa kwa pamoja huku kila lugha ikiwa imejikamilisha kisarufi katika kiwango hicho cha sentensi. Turejeelee mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 6 kwa ufafanuzi zaidi:

Jedwali Na. 6: Uchanganyaji wa Sentensi za Kiswahili na za Kiingereza

Na.	Uchanganyaji Msimbo katika Kiwango cha Sentensi	Tafsiri ya Sentensi za Kiingereza kwa Kiswahili
i.	Sidhani kama kuna kiongozi atatokea kama Mwl. Nyerere. <i>This was charismatic leader</i>	Huyu alikuwa kiongozi mwenye mvuto.
ii.	Ungekuwa hai hadi leo nadhani mfumo wa vyama vingi ungekuwa na thamani zaidi. <i>We miss you Nyerere.</i>	Tunakukumbuka Nyerere.
iii.	Mawazo yako yatatuongoza daima. <i>You are sorely missed.</i>	Unakumbukwa sana.
iv.	Pumzika kwa amani baba wa taifa. <i>We remember your slogan says 'Together We Can.'</i>	Tunakumbuka kaulimbiu yako inayosema 'Pamoja Tunaweza'.
v.	<i>This is the wisest president ever in East Africa.</i> Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.	Huyu ndiye rais mwenye busara aliyewahi kutokea Afrika Mashariki.
vi.	<i>I must admit that Tanzania had a leader</i> Mungu ailaze roho yake pema peponi.	Lazima nikiri kwamba Tanzania ilikuwa na kiongozi.
vii.	<i>Best president ever.</i> Nani yuko nami 2020?	Rais bora milele
viii.	<i>May his soul continue to rest in peace.</i> Baba hakuwa tu mwalimu ila alikuwa na kipawa cha unabii wa siasa.	Roho yake iendelee kupumzika kwa amani

Chanzo: Uwandani (2022)

Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 6, mawasiliano yamefanyika kwa kutumia mchanganyiko wa sentensi za Kiswahili na Kiingereza. Ingawa watafiti wengine hufasili matumizi hayo ya lugha kama ubadilishaji msimbo (Shartiely, 2016; Muyuku, 2017; Msovela, 2017), katika utafiti huu matumizi ya sentensi mbili au zaidi za lugha tofauti yamefasiliwa kuwa uchanganyaji msimbo. Fasili hii ni kutokana kwamba lugha mbili zimetumiwa katika kueleza au kufafanua mada ileile. Katika Jedwali 6(i-iv), ujumbe kuhusu Mwalimu Nyerere umetolewa kwa kuanza na sentensi za Kiswahili kisha kufuatiwa na za Kiingereza. Mathalani, tukirejeelea mfano 6(i), mtoamaoni anachanua hisia zake kwa kuanza na sentensi ya Kiswahili kwamba "Sidhani kama kuna kiongozi

atatokea kama Mwl. Nyerere.” Sababu ya maoni yake hayo anaitoa kwa kutumia sentensi ya Kiingereza kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi mwenye mvuto (*This was charismatic leader*). Vivyo hivyo, mtoamaoni mwingine anaanza kutoa maoni yake kwa kutumia Kiswahili katika 6(ii) kwamba Mwalimu Nyerere angekuwa hai mfumo wa vyama vingi ungekuwa na thamani zaidi. Kisha anafafanua zaidi kwa Kiingereza kwamba tunakukumbuka sana (*We miss you Nyerere*).

Katika 6(iii), mtoamaoni anatoa ujumbe wake kwa kuanza na sentensi ya Kiswahili kwamba ‘Mawazo yako yatatuongoza daima’ kisha anagubua hisia zake kwa sentensi ya Kiingereza kwamba wanamkumbuka sana Mwalimu Nyerere (*You are sorely missed*). Kutokana na mazuri aliyoyafanya kiongozi huyo hadi kupewa jina la Baba wa Taifa, katika 6(iv) ujumbe unatolewa kwa Kiswahili kuwa apumzike kwa amani. Kisha sentensi ya Kiingereza imetumiwa kutoa ujumbe kwamba wanakumbuka kaulimbiu yake inayosema ‘Pamoja Tunaweza’ (*We remember your slogan says “Together we can”*). Kwa ujumla, katika mifano tuliyoirejelea maelezo kuhusu sifa za Mwalimu Nyerere yametolewa kwa kuanza na sentensi za Kiswahili kisha kufuatiwa na za Kiingereza. Aidha, kila lugha imejikamilisha kisarufi katika sentensi husika.

Kwa upande mwingine, katika Jedwali 6(v-viii) ujumbe kuhusu Mwalimu Nyerere umetolewa kwa kuanza na sentensi za Kiingereza kisha kufuatiwa na Kiswahili. Tukirejelea mfano 6(v), sifa za kiongozi huyo zimetolewa kwa Kiingereza kwamba ‘Huyu ndiye rais mwenye busara aliyewahi kutokea Afrika Mashariki’ (*This is the wisest president ever in East Africa*). Mtoamaoni mwingine katika 6(vi) anakiri kwamba Tanzania ilikuwa na kiongozi (*I must admit that Tanzania had a leader*). Baada ya sifa hizo chanya, sentensi za Kiswahili zimetumiwa kutoa ujumbe wa kumwomba kwa Mungu kwamba roho yake ailaze mahala pema peponi. Katika 6(vii) ujumbe unatolewa kwa lugha ya Kiingereza kwamba Nyerere ni rais bora milele (*Best president ever*), kisha mtoamaoni anatafuta watu wengine wanaomuunga mkono kwa kuuliza kwa Kiswahili kama kuna mtu mwingine ana maoni kama yake (Nani yuko nami 2020?). Katika mfano wa 6(viii), ujumbe unaanza kutolewa kwa Kiingereza kwamba roho yake iendeleo kupumzika kwa amani (*May his soul continue to rest in peace*). Baada ya kumtakia mema huko aliko, sifa zake zinaendelea kuchanuzwa kwa Kiswahili kwamba hakuwa tu mwalimu bali alikuwa na kipawa cha unabii wa siasa.

Kwa kurejelea mifano hiyo, tunaona kuwa maoni yametolewa kwa kuchanganya sentensi za Kiingereza na Kiswahili. Aidha, kila sentensi imejikamilisha kisarufi katika lugha husika. Kwa kuangazia matumizi hayo ya lugha, yaani uchanganyaji msimbo katika kiwango cha sentensi, tunaweza kusema kwamba lugha zote mbili zimekamilishana katika kutoa ujumbe, yaani ni lugha msingi kwa upande mmoja na lugha changiaji kwa upande mwingine. Matokeo haya yanatofautiana na ya Msovela (2017), Shoo (2019) na Dzahene-Quarshie na

Sosoo (2023). Katika tafiti hizo, Kiswahili kimedhihirika kuwa msingi wa mawasiliano katika mitandaopepe. Hata hivyo, jamiilugha mtandao zilizohusishwa katika tafiti hizo sio changamani kama za kwenye mtandaopepe wa *YouTube*.

4.0 Hitimisho

Matumizi ya lugha katika mawasilianopepe yametawaliwa na wingilugha. Kutokana na hali hiyo, uchanganyaji msimbo umekuwa suala la kawaida katika muktadha huo. Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazotumiwa katika mawasilianopepe kwa kuchanganywa na lugha zingine, hususani Kiingereza. Lugha hizo mbili, yaani Kiswahili na Kiingereza, zimetumiwa kwa kuchanganywa katika mawasilianopepe ya jamiilugha changamani za kimtandao. Kwa kutumia Kiolezo cha Myers-Scotton (2001) kinachohusu uchanganyaji msimbo, wakati mwingine Kiswahili kimekuwa msingi wa mawasiliano na vipashio mbalimbali vya Kiingereza vimetumiwa kukamilisha mawasiliano hayo. Katika baadhi ya miktadha, Kiingereza kimetumiwa kama msingi wa mawasiliano na Kiswahili kujaliza sarufi ya lugha hiyo. Lugha hizo zimetumiwa kwa pamoja katika baadhi ya miktadha huku kila moja ikijikamilisha kisarufi. Matumizi haya ya lugha yanatupa dokezo kwamba wapo wawasiliani wenye uelewa wa lugha zote mbili kiasi cha kuzitumia kwa viwango sawia ingawa sio kwa wakati wote. Hali hii ni kutokana na uchangamani wa jamiilugha yenyewe kwani hujumuisha watu kutoka maeneo na matabaka mbalimbali na pia watu wenye umahiri tofauti wa lugha. Hivyo, wapo watu wanaofahamu Kiswahili zaidi kuliko Kiingereza na kinyume chake. Pia, wapo mahiri wa lugha zote mbili kiasi cha kuzitumia katika viwango sawia.

Marejeleo

- Abdallah, M.S. (2018). Chimbuko la Lugha Tandawazi kutumika katika Kiswahili Sanifu na Athari zake kwa Jamii. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Abdullah, D., Sastraatmadja, A.H.M., Lestari, N. C., Saputra, N. na Al Haddar, G. (2023). "Implementation of Youtube as a Learning Media in the New Normal Era". *Cendikia: Media Jurnal Ilmiah Pendidikan*. 13(3): 476-481.
- Abusa'aleek, A.O. (2015). "Internet Linguistics: A Linguistic Analysis of Electronic Discourse as a New Variety of Language". *International Journal of English Linguistics*. 5(1): 135-145.
- Alzubi, A.M. (2022). "Impact of Digital Media on Conventional Media and Visual Communication in Jordan". *Journal of Engineering, Technology and Applied Science*. 4(3): 105-113.
- Arkan, F. na Fahmi, A.T. (2022). "The Use of Slang in YouTube Comments". *Journal of English Teaching and Applied Linguistics*. 2(1): 23-26.
- Baumann, L. na Utz, S. (2021). "Professional Networking: Exploring Differences Between Offline and Online Networking". *Journal of Psychosocial*

- Research on Cyberspace*. 15(1). Article 2. <https://doi.org/10.5817/CP2021-1-2>
- Benard, T.M.; Kandagor, M. na Opijah, A. (2017). “Mitindo ya Lugha Ibuka katika Mitandao ya Kijamii: Mifano kutoka Mawasiliano ya Facebook”. *MULIKA*. Toleo Maalumu: 157-174.
- Benson, P. (2015). “Commenting to Learn: Evidence of Language and Intercultural Learning in Comments on YouTube Videos”. *Language Learning and Technology*. 19(3):88-105.
- Boyd, M. (2014). (New) “Participatory Framework on YouTube? Commenter Interaction in US Political Speeches”. *Journal of Pragmatics*, <http://dx.doi.org/10.1016/j.pragma.2014.03.002>
- Bridges, A.W. (2016). “Skills, Content Knowledge, and Tools Needed in a 21st Century University-level Graphic Design Program”. *Visual Communication Journal*. 52(2): 1-12.
- Chacha, D.M. (2002). “Julius Nyerere: The Intellectual Pan-Africanist and the Question of African Unity”. *AJIA*. 1&2: 20-39.
- Crystal, D. (2006). *Language and Internet*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Dzahene-Quarshie, J. na Sosoo, F.K. (2023). Language Blending in Tanzanian Adverts: Codeswitching between Swahili, English, and Kiswahili cha Mtaani. *Legon Journal of the Humanities*. 34(1): 118-152.
- Faki, M.H. (2018). Matumizi ya Lugha Tandawazi katika Mitandao ya Kijamii, Changamoto katika Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamivu (Haijchapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Fedeo, I. (2021). “Nyerere in the Eyes of his Critics”. *Journal on Interdisciplinary Studies in Humanities*. 4(1): 46-57.
- Harya, T.D. (2018). “Sociolinguistics: Code Switching and Code Mixing”. *Jurnal Ilmiah Kependidikan*. 11: 87-98
- Jagero, J., Mohochi, E. na Indede, F. (2013). “The Usage of Kiswahili in Blog Discourse and the Effect on its Development”. *International Journal of Humanities and Social Science*. 3(14): 192-200.
- Kandagor, M. (2020). “The Place of Kiswahili in the Twenty-First Century”. Katika J.R. Chepyator-Thomson, A. Ojo, K. Sonkeng na K. Traore (Wah.), *Youth, Globalization, And Society in Africa and its Diaspora*. Newcastle: Cambridge Scholars Publishing. Kur. 114-124.
- Kim, D.H., Week, B.E., Lane, D., Hahn L.B. na Kwak, N. 2021. “Sharing and Commenting Facilitate Political Learning on Facebook: Evidence From a Two-Wave Panel Study”. *Social Media and Society*. 7(3): 1–11.
- Landert, D. (2017). “Participation as User Involvement. Katika C.R. Hoffman na W. Bulblitz (Wah.), *Pragmatics and Social Media*. Berlin: Mouton de Gruyter. Kur. 31-57.

- Mabule, D.R. (2015). "What is This? Is it Code Switching, Code Mixing or Language Alternating". *Journal of Educational and Social Research*. 5(1): 339-350.
- Meliani, P.E., Ratminingsih, N. na Mahendrayana, G. (2021). "Code Mixing as Language Style in Communication through Social Media Twitter". *Journal of English Language Education*. 4(2): 91-101.
- Myers-Scotton, C. (2001). "The Matrix Language Frame Model: Development and Responses". *Trends in Linguistics Studies and Monographs*. 126: 23-58.
- Mnenuka, A. (2013). "Uambishaji wa Vitenzi vya Kiingereza katika Kiswahili: Mifano kutoka Mitandao ya Kijamii ya Kielektroniki". *Journal of Linguistics and Language in Education*. 7(1): 48-63.
- Mnenuka, A. (2019). "Utendajipepe wa Fasihi Simulizi: Haja ya Kuwa na Tawi Jipya". *Eastern African Literary and Cultural Studies*. 5(3-4): 170-190
- Mnenuka, A. (2024). "Is This Language Standard?" A General Survey on Swahili Computer-Mediated Communication. *Journal of Linguistics and Language in Education*. 18(1): 18-34.
- Monderin, C.P. na Go, M.B. (2021). "Emerging Netspeak Word Choices in Social Media on Filipino Pop Culture". *International Journal of Linguistics, Literature and Translation*. 4(6):49-61.
- Moshi, L. (2006). *The Globalized World Languages: The Case of Kiswahili*. Selected 12 Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics, ed. Olaoba F. Arasanyin and Michael A. Pemberton, pp. 166-175. MA: Cascadilla Proceedings Project.
- Msovela, S. (2017). *Analysis of Code-Switching in Social Media Chats among English-Swahili Bilinguals: A Case of Jamii Forum*. Tasnifu ya Umahiri (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mustikawati, D.A. (2016). "Code-Mixing and Code Switching in the Process of Learning". *Register Journal*. 9(1): 24-51.
- Mutembei, A.K. (2011). "Kukitandawazisha Kiswahili kupitia Simu za Kiganjani: Tafakari kuhusu Isimujamii". *Swahili Forum*. 18: 198-210
- Muyuku, J.A. (2017). "Codeswitching in Newspaper Discourse: A Case of Crazy Monday Articles in the Standard Newspaper". *Baraton Interdisciplinary Research Journal*. 7: 1-8.
- Ndekiro, R. (2020) "Sababu za Matumizi ya Lugha Tandawazi katika Mtandao wa Facebook na Athari zake katika Kiswahili Sanifu". *MULIKA*. 39: 147-158.
- Plonski, P.; Teferra, A. na Brady, R. (2013). *Why are More African Countries Adopting English as an Official Language? Makala iliyowasilishwa katika Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya ya Masomo ya Kiafrika (African Studies Association), Novemba 23, 2013, Baltimore, Malyland.*
- Radhaswati, D.A.A. na Nitiasih, K.N. (2022). "The Appearances of Code Switching and Code Mixing in Online Conversation". *Lingua Scientia*. 29(2):86-99.

- Rutechura, F. (2018) "The Discourse of Conflict in Social Media Networks". *UTAFITI*. 13(1): 93-102.
- Sanga, I.S. (2020). "Julius Nyerere's Understanding of African Socialism, Human Rights and Equality". *The Journal of Social Encounters*. 4(2):14-33.
- Saragih, M.Y. and Harahap, A.I. (2020). "The Challenges of Print Media Journalism in the Digital Era". *Budapest International Research and Critics Institute*. 3(1): 540-548.
- Shartiely, N.E. (2016). "Code-Switching in University Classroom Interaction: A Case Study of the University of Dar es Salaam". *Stellenbosch Papers in Linguistics Plus*. 49:215-231 doi: 10.5842/49-0-663
- Shiryayeva, T.A., Arakelova, A.A., Tikhonova, E.V., Mekeko, N.M. (2020). "Anti-, Non-, and Dis-: the Linguistics of Negative Meanings about YouTube." *Heliyon*. 6:1-9.
- Shoo, V.M. (2019). Multilingualism in Computer Mediated Communication. A study of Language Choice among Youngsters in Rural Tanzania. Tasnifu ya Umahiri (Imechapishwa). Chuo Kikuu cha Inland, Norway.
- Strangelove, M. (2010). *Watching YouTube: Extraordinary Videos by Ordinary People*. Toronto: Toronto Press.
- Tabe, C.A. (2023). "Code-Mixing and Code-Switching in Cameroon Social Media". *International Journal of Linguistics and Translation Studies* 4(1).47-61. <https://doi.org/10.36892/ijlts.v4i1.279>
- Yusnida, D., Muliawati, I. na Rezeki, H.S. (2022). "A Descriptive Analysis of Code-Mixing Types Used by Youngsters in Online Communication". *Journal of English Teaching and Linguistics*. 3(2): 98-108.
- Waris, M.A. (2012). "Code Switching and Mixing". *Jurnal Dakwah Tabligh*. 13(1): 123-135